"KIZIDUO"

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE**

# MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI (CMT) CHA TAREHE 13.10.2021 KUPITIA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI ROBO YA KWANZA (1) MWEZI JUNI HADI SEPTEMBA 2021

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| NA | JINA LA MJUMBE | CHEO |
|---|---|---|
| 1 | EVELINE P. MERAY | KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI |
| 2 | ENG MASOTA MALULU | KAIMU MKUU WA IDARA YA UJENZI |
| 3 | ALLY O NCHURIKA | KAIMU MKUU WA IDARA YA MAZINGIRA NA UDHIBITI WATAKA NGUMU |
| 4 | MOHAMMED LUNGIA | KAIMU MKUU WA IDARA YA FEDHA NA BIASHARA |
| 5 | SAADI S. NYAGAWA | MKUU WA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI |
| 6 | ANTHOMY K. DANIEL | KAIMU MKUU WA IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI |
| 7 | JITIHADA AMON | KAIMU KATIBU TSC |
| 8 | DKT RIO ERNEST | KAIMU MKUU IDARA YA AFYA |
| 9 | BAKARI MALIMA | MKUU WA IDARA YA KILIMO, USHIRIKA NA UMWAGILIAJI |
| 10 | ANDREW A. MITUMBA | KAIMU MKUU WA IDARA YA ELIMU MSINGI |
| 11 | DICKSON MWENDA | KAIMU MKUU WA IDARA YA ARDHI NA MALIASILI |
| 12 | ISIHAKA I. MWALIMU | MKUU WA IDARA YA ELIMU SEKONDARI |
| 13 | ANDREW GREGORY | MKUU WA KITENGO CHA SHERIA |
| 14 | HAULE PETER MWAMSIKU | KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MTHIBITI UBORA WA ELIMU |
| 15 | AMEDEUS MBUYA | KAIMU MKUU WA KITENGO CHA TEHAMA |
| 16 | MALIFIMBO MALIFIMBO | MKUU KITENGO CHA MANUNUZI |
| 17 | GODFRID NKUBA | MKUU WA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII |

**SEKRETARIETI**

| NA | JINA LA MJUMBE | CHEO |
|---|---|---|
| 1 | SIBONIKE LAZARO | Katibu wa Vikao |

## AGENDA NA.KTV/MPDC/01/29/04/2021: KUFUNGUA KIKAO

Katibu alieleza kuwa akidi inayotosheleza kuanza kikao imetimia, hivyo Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Kikao. Mwenyekiti alianza kwa kuwapongeza, Kisha alifungua kikao saa 06:50 mchana.

## AGENDA NA.KTV/MPDC/02/29/04/2021: KURIDHIA AGENDA.

Katibu aliwasilisha jumla ya agenda 12 kwa Wajumbe

1. Kufungua Kikao
2. Kuridhia Agenda
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 06.07.2021.
4. Kusoma na kuthibitisha yatokanayo na kikao cha tarehe 06.07.2021.
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwezi Julai, Agosti na Septemba 2021
6. Taarifa ya manunuzi ya mwezi Julai, Agosti na Septemba 2021.
7. Taarifa za fedha za iCHF na NHIF kwa mwezi Julai, Agosti na Septemba 2021.
8. Kutoka vituo vya huduma za Afya

9. Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara.
   a) Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji
   b) Idara ya Elimu Sekondari.
   c) Kitengo cha TEHAMA.
   d) Kitengo cha Nyuki
   e) Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi.
   f) Idara ya Ujenzi
   g) Idara ya Utawala na Utumishi.
10. Taarifa ya mapokezi ya fedha ya maendeleo UVIKO 19
11. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai, Agosti na Septemba 2021.
12. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti.
13. Kufunga Kikao.

Wajumbe waliridhia Agenda zote zilizowasilishwa.

**AGENDA NA.KTV/MPDC/10/29/04/2021: - TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS.1,370,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA MIRADI YA MAENDELEO YA UVIKO 19**

Mwenyekiti alitoa taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya UVIKO kiasi cha Tshs. 1,370,000,000.00 miradi ambayo inatakiwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo;

1. Ujenzi wa madarasa 18 kwa shule shikizi
2. Ujenzi wa madarasa 31 kwa shule za Sekondari
3. Ujenzi wa Nyumba ya mtumishi (Three in one) Hospital ya Wilaya
4. Ujenzi wa jengo la dharula ya wagonjwa (EMD) Hospital ya Wilaya

Mwenyekiti alieleza kuwa fedha hiyo inatakiwa kutekelezwa kwa muda mfupi kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi na huduma nyingine kuweza kupatikana kwa wakati, na pia njia iliyopendekezwa ya utekelezaji ni kwa njia ya kuwatumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (Force Account) Hivyo kinachotakiwa ni kila idara husika kujipanga kwa ajili ya kutoa taarifa na kuutambulisha mradi kwa maeneo husika kwa ajili ya utekelezaji.

Wajumbe kwa pamoja walishukuru sana taarifa hiyo ya upokeaji wa fedha na kusema kuwa itapelekea kwenda kupunguza adha mbalimbali ambazo zinatukabili hasa ya upungufu wa madarasa.

**AGENDA NA.KTV/MPDC/12/12/2021 KUFUNGA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha mwenyekiti ili afunge kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao, na kusisitiza kila Mkuu wa Idara na Kitengo kuendelea kusimamia kikamilifu shughuli za Idara na Kitengo kulingana na mpango na maelekezo yaliyotolewa katika kikao hicho, Kisha alifunga kikao saa 08:52 mchana.

**Muhtasari Umethibitishwa na Kusainiwa na:**

| | |
|---|---|
| Saini ya Katibu | Saini ya Mwenyekiti |
| [signature]........ | [signature] |
| **Ignas Tadeo** | **Catherine M. Mashalla** |
| Tarehe: 13/10/2021... | Tarehe: 13/10/2021.. |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KWA MWAKA (2020/2021) KILICHOKETI TAREHE 27 OCTOBA, 2021.
## MUHTASARI NAMBA: TB: 4/2020/2021

**WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Godfrid P. Nkuba | Afisa Maendeleo ya jamii (W) | Mwenyekiti |
| 2. Malifimbo L. Malifimbo | Afisa ugavi (W) | Katibu |
| 3. Andrew Gregory | Mwanasheria | Mjumbe |
| 4. Anthon Daniel | Afisa Mipango | Mjumbe |
| 5. Martin Lohay | Mganga Mkuu | Mjumbe |
| 6. Andrew Mitumba | Afisa Elimu Msingi | Mjumbe |

**B. SEKRETARIETI.**

1. Hipolite S. Gimeno

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/01. KUFUNGUA KIKAO**

Baada ya kujiridhisha na akidi, Mwenyekiti alifungua Kikao saa 12:51 Mchana, kwa kuwataka Wajumbe wajielekeze kwenye mjadala mzima wa agenda ambazo ziliwasilishwa mbele yao.

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/02. KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.**

Jumla ya Agenda saba **(7)** ziliridhiwa ili zijadiliwe. Agenda hizo ni:-

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda za Kikao
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 12 Julai, 2021.
4. Kuridhia ujenzi wa miradi ya COVID kwa kutumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (ujenzi wa force)
5. Mengineyo.
6. Kufunga Kikao.

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/3 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 12 Julai, 2021.**

Muhtasari wa Kikao kilichofanyika tarehe 12 Julai, 2020, ulisomwa, ambapo Wajumbe waliafiki kuwa, yote yaliyomo kwenye Muhtasari huo ndio waliyoyajadili na kuyatolea maamuzi. Kuthibitisha hayo, Mwenyekiti na Katibu waliweka saini zao kwa niaba ya wote, ili Muhtasari huo uwe kumbukumbu halali wa Kikao hicho.

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/4 KUPITISHA MANUNUZI NA UJENZI WA MIRADI YA MADARASA YA SEKONDARI NA MSINGI NA MIRADI YA AFYA YA UVIKO KWA KUTUMIA MAFUNDI WASIOKUWA WAKANDARASI (FORCE ACCOUNT) YENYE GHARAMA TSHS. 3,650,000.00**

Katibu aliwaeleza majumbe kuwa kuna fedha imepokelewa za COVID 19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya sekondari 31, madarasa ya shule shikizi 18, ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Three in one) moja na jengo la huduma ya dharura kati hospitali ya wilaya. Hivyo aliwaomba wajumbe waridhie miradi hiyo ikatekelezwe kwa kutumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (Force Account) kwa kuwa hayo ni matakwa ya mfadhili wa miradi.

**AZIMIO**

Wajumbe walikubaliana kwa Pamoja na kuridhia kuwa kazi hiyo ikafanyika kwa kutumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (Force Account) na wajumbe walishauri kuwa ni vizuri miradi hii itambulishwe haraka kwenye ngazi za huko shuleni ili miradi iweze kutekelezwa kwa wakati

**AGENDA NA:TB 04/2019/2020/5. MENGINEYO.**

**Hakukuwa na mengineyo**

**AGENDA NA:TB 04/2019/2020/6. KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga Kikao saa 08:20 mchana na alitumia fursa hiyo kuwashukuru Wajumbe kwa michango yao.

| **MUHTASARI** | **UMETHIBITISHWA** |
|---|---|
| ..........[signature].......... | ..........[signature].......... |
| **Malifimbo L. Malifimbo** | **GODFRID P. NKUBA** |
| KATIBU WA BODI YA ZABUNI | MWENYEKITI WA BODI YA ZABUNI |

..........27/10/2021..........

**TAREHE.**